

## **TOFAUTI KATI YA KUJAZWA ROHO MTAKATIFU NA KUJAWA NA ROHO MTAKATIFU.**

### **1. Kujazwa Roho Mtakatifu: Filled with the Holy spirit**

**Mdo. 2:4-** Ni kupokea Roho Mtakatifu kwa mara ya kwanza na kunena/kusema kwa lugha nyingine – lengo hasa la kunena kwa lugha kwa mara ya kwanza ni **kuijenga** nafsi ya mtu ambayo ilikuwa **imebomolewa** na mambo mengi mno ya dunia hii kabla ya kuokoka. **1Kor. 14: 2 – 4.** Roho Mtakatifu **anakalia** (anatawala) na kwanza kumwongoza na kumfundisha mtu – **Rumi 8: 14, Yoh. 16: 12 – 14.**

### **2. Kujawa Roho Mtakatifu – (Full of the Holy Spirit)**

Mtu anajawa na tabia ya kudumu katika uwepo mkamilifu wa Mungu wakati wote hata kama anapambana na mazingira hatarishi. (yaani baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu ukatembea kwa uaminifu na Mungu ukiongozwa na Roho Mtakatifu ndipo inaumbika ndani yako tabia ya kudumu katika uwepo wa Mungu wakati wote (**huku ndiko kujawa na Roho Mtakatifu.**) Wewe unatembea kwa uaminifu katika hali zozote zile na matendo ya mwili yanafishwa kabisa ndani yako hata kama uko peke yako au unapitia mazingira magumu. **Mdo. 6:3, 5: 27-33, 40-42, 7:54 – 60, Mwanz. 39: 6 – 12, Dan. 3: 15 - 22, 6:10 –**

- **Kazi kubwa ya** Roho Mtakatifu ndani yetu ni pamoja na **kuyafisha** matendo ya mwili huu!! **Rum. 8: 12 – 13**

**Note: Yesu Kristo aliwatokea watu tofauti tofauti mara 11 baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu ndani ya siku 40.**

1. Mariamu Magdalena - **Yoh. 20: 11 – 18**
2. Petro binafsi - **Luk. 24: 34**
3. Cleopa na mwenzake – **Luk. 24: 13 – 35**
4. Wanafunzi wake wote Kasoro Tomaso **Luk. Luk.24:36 – 43**
5. Wanafunzi wake wote siku ya Jumapili –**Yoh. 20: 26 – 31**
6. Wanafunzi wake 7 tu kando ya Bahari ya Galilaya - **Yoh.21: 1 – 25**
7. Watu mia tano huko Galilaya – **1kor. 15: 6**
8. Yakobo ndugu yake na Yesu – **1Kor. 15: 7**
9. Wanafunzi wake wote wakati wa kupokea agizo kuu la kwenda kuhubiri Injili duniani kote. **Math. 28: 16- 20**
10. Mitume na wanafunzi wake wote (120) wakati wa Yesu anapaa (mlima wa Mizeituni – **Mdo. 1:3 – 11** na mwisho
11. Mtume Paulo - **1Kor. 15:8 (Mdo. 9: 1 – 9)**

**NA**

**Askofu Dr. L. Mwizarubi**

**2021**